# *KUIELEZEA HUDUMA*

Asante, Ndugu Demos.

2 Sina shughuli yoyote hapa, ama kuchukua wakati wa Ndugu Brown na wengineo, lakini ninaifurahia fursa ya kuwa Phoenix. Na ni, hakuna njia kwangu kuelezea jinsi ninavyojisikia kwa watu hapa Phoenix, waliokusanyika humu: kama nifanyavyo watu kila mahali. Na ushirika ambao tumekuwa nao juma hili, ama, juma lililopita, hasa, miongoni mwa makanisa hayo huko nje, nilipata kutembelea makanisa kumi mbalimbali, madhehebu matatu ama manne mbalimbali, na huo ushirika miongoni mwa ndugu bila shaka ulikuwa mzuri mno. Ninakumbuka wakati Ndugu Williams alipopitia hapa, ninaamini alikuwa tu akishuka kutoka kwa Mayo, nasi tulikuwa na muda kidogo pamoja.

3 Sasa, tukizungumza juu ya mkutano huu, nami nimezungumza mara nyingi na Wafanyabiashara, mtu fulani aliniambia wakati mmoja, kasema, "Aisee, wewe ni mhubiri. Kwani una shughuli gani na wafanyabiashara?"

Nikasema, "Mimi ni mfanyabiashara."

Basi kasema, "Unafanya biashara ya aina gani?"

Nikasema, "Bima...Dhamana. Bima ya maisha." Kama mtu yeyote anataka hati ya mkataba, ningetaka kuizungumzia pamoja nawe baada ya ibada.

4 Wakala mmoja wa bima, wakati mmoja alikuja nyumbani kwangu, nasi tulikuwa marafiki wakubwa pamoja, tulisoma naye shuleni, na jina lake ni Wilmer Snyder, huenda ameketi hapa usiku wa leo. Kwa hiyo akaniambia, akasema, "Billy, ningetaka kukuhamasisha kwa hati ya bima."

5 Vema, nilikuwa na maskini hisia ngeni juu yake. Nami... Si kumhusu yeye, bali ni huko kuyawekea bima maisha yangu, tayari yana bima. Kwa hiyo nikasema, "Wilbur," nikasema, "Sina bima yoyote kama *hiyo*, sidhani." Nikasema, "Nina ninii, hati moja ya mkataba," nami nikasema, "Ninaamini hiyo itatosha."

Naye akasema, "Loo, tayari una bima, Billy?"

Nami nikasema, "Naam, uh-huh."

Ndipo mke wangu akaniangalia kote kana kwamba anasema, "Kwani imekuwaje kwake?"

Kisha kasema, "Kuwa na...Una bima ya aina gani, Billy?"

Nikasema, "Hakikisho lililobarikiwa, Yesu ni Wangu."

Naye akasema, "Billy, hiyo haitakuweka hapa juu makaburini."

6 Nikasema, "Itanitoa, sina wasiwasi kuhusu kuingia mle, la, la." Sina wasiwasi kuhusu kuingia mle, nitakuwa mle, ni kutoka tu.

7 Kwa hiyo hati hii ya mkataba ninayozungumzia . . . Kwa hiyo mimi ni mfanyabiashara, nina furaha sana kushirikiana na watu hawa ambao wana . . . wanabeba hati ile ile: bima ya Uzima wa Milele.

8 Na sasa, jana ilikuwa ndiyo mara ya kwanza niliyowahi kujaribu kuona kwamba Roho Mtakatifu angenena katika mojawapo ya mikutano hii. Nami nitawaambia ni kwa nini. Tuko kule tumestarehe tu, na kupaza sauti, na kupiga makelele na hao wengine, tukiwa na wakati mzuri, na kwa namna fulani ni vigumu basi, kwa kawaida, katika ibada kama hizo, mimi sili, labda, kwa siku moja ama mbili, huja kwenye ibada na kusimama pale. Ni jambo lisiloeleweka, hata hivyo, najua linatoka kwa Mungu, nina hakika ya hilo, kwamba linatoka kwa Mungu.

9 Kama mvulana mdogo, nilipozaliwa mara ya kwanza, mmesoma hadithi yangu, jinsi Nuru ilivyokuwa ikining'inia juu ya kitanda kidogo nilimozaliwa. Mama yangu, baba, hawakujua lolote kwamba Hiyo ilikuwa ni nini. Na baadaye, nilipokuwa tu jamaa mdogo, ilinena nami na kusema, "Kamwe usinywe pombe," ilininii tu . . . "au kuvuta sigara, au kujitia unajisi kwa njia yoyote. Kuna kazi ya kufanya utakapokuwa mtu mzima." Ikaendelea. Nao watu wangu walidhani labda . . .

Wakati maono yalipoanza kutokea mbele yangu kwa mara ya kwanza, mbona, ningeenda nikamwambia mama yangu, "Unajua, ni—niliona ja—jambo *fulani-fulani* likitukia."

Angesema, "Billy, ulilala usingizi."

"La, mama, sikulala." Nasi tungeona, yalitukia vivyo hivyo hasa.

10 Na, marafiki zangu Wakristo, hatujui kamwe mkutano wetu wa mwisho utakuwa lini. Kama tukikutana hapa mwaka ujao, natumaini tutakutana, lakini hapana shaka baadhi yetu hawatakuwa hapa, itatubidi kuondoka kabla ya mwaka ujao, katika kundi la watu wengi hivi, ambamo kuna magonjwa, na wazee, na kadhalika. Nasi sote hatuna budi kukutana na ushuhuda wetu Huko tena, kwa hiyo hatuna budi kuwa waaminifu.

11 Ninathamini yale Ndugu Ford aliyosema dakika chache zilizopita, "Kuna Kitu kimoja tu kilicho sahihi, na hicho ni Neno la Mungu." Hiyo ni kweli kabisa, dumuni moja kwa moja na Hilo; basi, "Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu ndani yenu, basi ombeni mtakalo."

12 Sasa, hivi ndivyo ilivyoonekana daima kwangu, enyi marafiki: kwamba, kama Mungu aliwahi kuwa Mungu, Yeye

angali ni Mungu, na kama halitimizi Neno Lake, basi kuna, hakuna kitu Kwake.

13 Kama vile jamaa mdogo, wakati mmoja, alienda chuoni kujifunza kuwa mhudumu. Na alipokuwa ameondoka, mamaye akashikwa na ugonjwa mbaya sana, naye akatuma habari chuoni kumfanya mvulana huyo arudi nyumbani, kwa sababu walidhani huyo mama atakufa, halafu kesho yake asubuhi, telegramu nyingine ikaja, ikasema, "Hajambo."

14 Yapata mwaka mmoja baadaye, mvulana huyo akatembea nyumbani, akasema, "Mama, ningetaka kujua kile daktari alichokufanyia, na kwamba huyo daktari alikuwa ni nani. Hicho ndicho kisa cha haraka sana cha nimonia nilichopata kujua kikiponywa."

Naye akasema, "Loo, Mwanangu," kasema, "haikuwa ni daktari," kisha kasema, "tena, ilikuwa ni Daktari."

Kasema, "Jina lake lilikuwa nani?"

Kasema, "Dk. Yesu."

Basi kasema, "Mbona, unamaanisha Yesu, aliye Kristo?"

Kasema, "Ndiyo." Kasema, "Unajua lilipo maskini kundi lile dogo la watu kule chini kando ya barabara, lililo na ile misheni ndogo?"

"Naam."

15 Kasema, "Walikuwa wakifanya, wakikutana huko usiku mmoja, nao walikuwa na mkutano wa maombi. Ndipo daktari akaniambia ya kwamba nisingeweza kupona, mimi, nimekuwa hali mbaya sana." Kisha kasema, "Walisema walijisikia kuongozwa kuja kule na kuniombea." Ndipo akasema, "Unajua nini, Mwanangu?" Kasema, "Utukufu kwa Mungu, Yesu aliniponya."

Na kwa hiyo huyo mvulana akasema, "Mama, *tsk*, *tsk*, *tsk*, *tsk*, dhihaka. Mbona, hata unatenda kama wao. Hupaswi kufanya hivyo."

"Loo," akasema, "lakini, Mwanangu, liko moja kwa moja katika Biblia." Kasema, "Walinisomea moja kwa moja kutoka kwenye Biblia."

16 "Mbona," kasema, "Mama," kasema, "wewe—wewe... Hilo—hilo si sawa." Kasema, "Watu hao hawana elimu, hawaielewi Biblia." Kasema, "Tulijifunza mambo hayo chuoni." Kasema, "Hawaele-..."

Kasema, "Mwanangu, ngoja kidogo tu, niliyaandika." Akaenda pale na kusoma Marko 16, "'Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.'"

"Loo," akasema, "Mama, unafahamu kwamba tulijifunza chuoni Marko 16 kuanzia kifungu cha 9 na kuendelea hata haijavuviwa."

Akasema, "Haleluya! Haleluya!"

Akasema, "Mama, una shida gani?"

Kasema, "Nilikuwa tu nikiwazia, kama Mungu angeweza kuniponya kwa Neno *lisilovuviwa*, angeweza kufanya nini na Lile lililovuviwa kweli?"

Kwa hiyo, Ndugu Ford, ninaamini lote limevuviwa, na hiyo ndiyo kazi Yake.

17 Karibu nimetoka uwanjani kuiacha huduma, kwa sababu imenilemea mno nyumbani, watu wanatoka kila mahali. Wala hakuna kitu . . . Siwezi kujibunia ono, inahitaji Mungu kufanya hivyo.

18 Lakini hebu . . . Ni wangapi wenu ninyi watu mmewahi kuiona picha hiyo? Wameipiga picha mara nyingi sasa. Nadhani kuna mamia humu ndani walio nayo, ambayo imepitia Washington, DC, kupitia kwe—kwenye shirika la J. Edgar Hoover, George J. Lacy wa alama ya vidole ya FBI na hati. Imepigwa picha mara nyingi. Ni Nuru ndogo, karibu *ukubwa huu* kuzunguka, Nuru ya kaharabu, inayowaka. Na huyo Ndiye aliyezungumza nami sikuzote.

19 Na hebu tuchunguze tu nyuma. Endapo hiyo si ya Kimaandiko, basi achana nayo. Kama kamwe nikisema jambo lolote mbele zenu, kama Fundisho au ufafanuzi, ambalo haliko katika Biblia, lisahauni, kwa sababu si kweli. Na kama Malaika yeyote, sijali jinsi anavyoonekana halisi, na jinsi alivyovuviwa, kama akinena kinyume na Neno la Mungu, achaneni naye, yeye si wa Mungu. Wagalatia 1:8 ilisema, "Malaika kutoka Mbinguni akihubiri fundisho lingine lolote mbali na hili, lilivyo, yale yaliyofundishwa tayari, na alaaniwe." Ha—hatuchukui kitu ila kile tu Mungu . . .

20 Sasa, tunaona ya kwamba katika Biblia, wakati Mungu alipowaongoza wana wa Israeli kupitia nyikani . . . Sasa, sichukui wakati wa Ndugu Brown, natumaini. Lakini wakati . . . Ninajua ni vigumu, kuketi pale katika uchovu. Naye mhudumu anapaswa kuwa nje chumbani mahali fulani, kisha aje moja kwa moja mbele ya kusanyiko lake, kutoka kwenye utamu wa Mungu, na—na peke yake akisoma; nami najua ni vigumu.

21 Basi Mungu alipowaongoza wana wa Israeli kutoka Misri . . . Kumbukeni Malaika wa Agano alikuwa ni Nguzo ya Moto, sote tunajua hilo, Huyo alikuwa ni Malaika wa Agano, nasi tunajua ya kwamba Huyo alikuwa ni Yesu Kristo. Nasi tunaona ya kwamba Musa aliiacha Misri, akihesabu kushutumiwa kwake Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko ule Farao angeweza kumpa huko Misri.

22 Tunaona wakati Malaika huyu alipodhihirishwa, kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Alisimama duniani, tunazijua kazi alizofanya alipokuwa hapa duniani. Tunaona ya

kwamba ninii Yake. . . Yeye alikuwa awe Masihi, naye Masihi alikuwa na ishara ambayo ingemfuata Masihi, na hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya nabii, kwa kuwa Israeli daima walifundishwa kuwaamini manabii wao. Wakati alipokuwa hapa Yeye alisema, "Nalitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu."

23 Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Paulo alikuwa akienda zake Dameski, basi alipokuwa akishuka kwenda zake, alibwagwa chini na Nuru, Nguzo ya Moto. Sasa, kumbukeni, kwanza ilikuwa ni Nguzo ya Moto, kisha ikafanyika mwili, halafu ikarudi kwa Mungu, ndipo sasa, hapa Paulo anaiona. Hakuna hata mmoja wa hao wengine aliyeiona, ni Paulo tu.

24 Unajua, unaweza kuona vitu mara nyingi ambavyo wengine hawana chochote, hawawezi kuviona hata kidogo. Hao askari, ama wowote wale, walinzi wa hekalu waliokuwa pamoja na Paulo, hawakuiona Nuru hiyo, bali ilikuwa halisi sana kwa Paulo hata ikayapofusha macho yake. Ndipo Paulo akapaza sauti, akasema, yeye. . . Kwanza, Sauti ikasema kutoka kwenye Nguzo ya Moto, kasema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Naye akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Naye akasema, "Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kuupiga teke mchokoo." Ni wangapi waliowahi kusoma hayo? Hakika.

25 Ndipo alikuwa katika Roho, akadhihirishwa katika mwili kuondoa dhambi, Mungu, akarudi kwa Mungu, Roho. Na sasa, wanapopiga picha hii siku hizi, pamoja nasi, watu wa Bwana, na ni Nguzo ile ile ya Moto.

26 Sasa, njia pekee inayoweza kuthibitishwa ya kwamba ni Nguzo ile ile ya Moto: Itafanya kazi zile zile kama ni Nguzo ile ile ya Moto, Roho wa Mungu. Yesu alisema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo ninyi mtaniona Mimi. Kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Waebrania 13:8 ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Basi kama Roho huyu hazai Uzima wa Kristo, basi Yeye si Roho wa Mungu.

27 Sasa, kama nilisimama hapa nikiwa na makovu ya misumari mkononi mwangu, na—na alama za, kote kichwani mwangu hapa pamoja na. . . kutokana na taji ya miiba, na kuwaambia ya kwamba Roho wa Mungu alikuwa ndani yangu, hilo lisingelifanya kuwa kweli. Mikono yangu ingeweza kweli kuwa na makovu, hilo lisingekuwa ni ushahidi, lakini unapoweza kusema ya kwamba Roho wa Mungu yuko ndani yetu, basi kazi za Mungu zitadhihirishwa kupitia maisha yako.

28 Kwa maneno mengine, kama mti, kama mzabibu. . . Yeye ndiye Mzabibu, Yohana Mtakatifu 15, sisi ni matawi. Sasa, mzabibu hauzai tunda, ni matawi, bali yanapata nguvu zake kutoka kwa huo mzabibu. Sasa Yesu hana mikono yoyote duniani ila yako na yangu, hana yoyote, wala kinywa chochote duniani ila chako na changu, ndipo tunatiwa nguvu na Roho wa

Kristo, na kama Uhai ulio ndani ya Mzabibu uko kwenye tawi, hilo tawi litazaa matunda yaliyo katika huo Mzabibu, bila shaka, tunajua hilo, mara nyingi, mamia ya watu, wakitoka kila mahali, kutoka mataifa yote.

29 Sasa, kabla sijaketi chini, ningetaka kusema hivi: Mara nyingi watu huja namna hii: Kuna mtu hapa ndani mahali fulani usiku wa leo, inadhaniwa, alikuja nyumbani, si muda mrefu uliopita, kuwapa tu mfano mdogo, Ndugu Welch Evans, nadhani yuko hapa. Uko hapa, Ndugu Evans? Inua mkono wako endapo upo. Naam, *hapa* kwenye ukuta. Yeye huja, anaendesha gari kama maili mia saba, njia moja, kila Jumapili, wakati ninapohubiri maskanini. Moja kwa moja yapata safari ya maili elfu moja na mia tano Jumapili, kuanzia Jumamosi, anaenda, anarudi Jumatatu au Jumanne.

30 Alikuwa na gari jipya la abiria na mizigo, akalileta Louisville. Nao wananinii, walikuwa na genge kubwa la wizi huko Louisville. Nao wa—wangeiba magari, wanayapeleka Bowling Green, yapata maili mia moja na kumi na nane huko chini, wanayapeleka kwenye duka la rangi, wanayapaka rangi, wanayatorosha. Wala si lazima uwe na hati ya kuuza magari huko Kentucky, wanaondoa namba kwenye bloku na kukutengenezea hati. Na, loo, lilikuwa ni genge la kutisha sana.

31 Bw. Evans, bila kujua jambo hili, aliingia kwenye, kwenye Mkahawa wa Miller, akaliacha gari lake wazi, akaingia kwenye mkahawa; akarudi nje, kinasasauti chake, nguo zao, gari lao na kadhalika, vilikuwa vimeenda, yeye na Ndugu Fred Sothmann.

32 Ndipo basi, wakashauriana, hawakujua la kufanya, basi wakasema, "Hebu twende kwa Ndugu Branham." Wakaja pale nyumbani.

Nikasema, "Vema, sijui. Tutaomba tu."

33 Sasa, huenda mkawazia hili lingekuwa ni kosa, lakini kupiga magoti, kuomba, siwezi kulifanya litendeke, Mungu hana budi kulitenda. Siidhibiti, inanidhibiti. Mnaona?

34 Basi nikaona hilo gari barabarani, likielekea Bowling Green. Jamaa mdogo alikuwa akiliendesha, alikuwa amevaa koti la ovaroli, alikuwa na tai ya kahawia. Nikaanza kuomba, sawasawa tu na lile ono yule mtu aligeuka barabarani, huyo mtu alikuwa—alikuwa Mkristo, ndipo Roho Mtakatifu akamsimamisha, akamgeuza, basi nikamwona mahali alipoliegesha hilo gari, nikamwambia Bw. Evans, "Nenda mahali *fulani-fulani*, nawe utapata gari lako pale. Nawe ulikuwa ndiyo kwanza umelijaza tangi lako."

"Naam."

"Litakuwa karibu limetumika nusu, kwa sababu ameendesha yapata maili mia moja kwake."

35 Bw. Evans akageuka, akatoka mahali hapo, nilimshikilia pale kwa muda mpaka lile ono liweze kutimia. Bw. Evans, akienda zake kwa Bw. Sothmann, papo hapo kando ya barabara, akitoka Louisville, kote kote mpaka Jeffersonville, upande wa pili wa mto, aliegesha hilo gari mahali *hapo*, nalo lilikuwa limeegeshwa pale pamoja na funguo, na, mle ndani, tayari. Je, hiyo ni kweli, Bw. Evans? [Ndugu Evans anasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Maombi.

Ninataka kuwaambia, si lazima uone ono, lakini omba tu. Unaona? Roho Mtakatifu alimsadikisha mtu huyo na kumgeuza.

36 Jambo lile lile lilitukia huko chini, wakati huyu . . . Meksiko, kuhusu maskini yule mtoto mchanga kule, maskini yule mtoto mchanga aliyekufa usiku huo, yule mama mchanga niliyekuwa nikiwaambia habari zake, roho yake ilikuwa imeondoka. Jambo lile lile alilofanya Bwana wetu alipokuwa hapa duniani, wakati roho ya Lazaro ilipokuwa siku nne mahali fulani, bali kwa Roho Mtakatifu Yeye aliigeuza roho ya Eli- . . . , uh, Lazaro ikarudi.

37 Mara nyingi watu huja, na kila namna ya mambo, na kusema, wanauliza maswali haya mbalimbali. Hapa, wachache . . . Ndugu Fred Sothmann, ninaamini ninamwona amesimama pale mlangoni, alikuwa ndiyo kwanza . . . Jambo moja, kusudi mweze kuona ninalomaanisha.

38 Hatuamini katika kuchukua karama ya Mungu, na kufanya ubao wa uaguzi kutoka kwake. Hampaswi kufanya hivyo. Katika hali tu . . . Naye Mungu hatalitumia hivyo, inamhitaji Yeye kulitumia hivyo hata hivyo.

39 Baadhi ya marafiki walikuwa wakija kumwona, trela lilikuwa limefungwa, hakuwa na, asingeweza kupata funguo zake kwa siku mbili ama tatu, alikuwa tu amechanganyikiwa kwelikweli, watu walikuwa wanakuja. Akapiga simu, akasema, "Ndugu Branham, wakati mmoja wana wa Yese walikuwa huko nje wakiwatafuta nyumbu fulani, wala wasingeweza kuwapata, kwa hiyo wakashuka wakamwendea Samweli na kuuliza walikuwa wapi. Naye Samweli akawaambia ya kwamba wa—wale nyumbu walikuwa tayari wamerudi." Akasema, "Je, utamwomba Mungu kuhusu hizo funguo?"

40 Kasema, "Nenda kwenye chumba chako cha faragha," baada ya kuomba, "angalia kwenye sweta ndogo uliyokuwa umevaa siku chache zilizopita." Hizo hapo zile funguo. Mnaona? Ni kitu gani? Inamaanisha jambo hili moja, enyi marafiki: kwamba Mungu angali ni Mungu tu kadiri alivyowahi kuwa. Mnaona? Sasa, sisi—sisi hatuna budi kukabiliana na jambo hilo, hatuna budi kuamini hilo, hatuna budi kujua ya kwamba hiyo ni kweli.

41 Lakini karama hizo zitatenda kazi tu . . . Wala haiwezi kutenda kazi kupitia kwa mtu binafsi, inahitaji imani ya mtu mwingine kuitumia karama hiyo.

42 Yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, mbona wengi wao walikuwa wakimgusa, lakini *imani* ya mwanamke huyo ndiyo iliyomgusa. Na mnano wakati wa hiyo imani kumgusa, ilikuwa . . . Yeye kwa kweli hakumgusa, alimgusa Mungu, na hilo ndilo lililosababisha hayo matokeo.

43 Daima iko hivyo. Kama imani yako inaweza kumgusa, basi karama ya namna hiyo ni u—upambanuzi tu ambapo Mungu hujibia kupitia mtu binafsi. Ili kwamba ninyi . . . Wengi wenu mliinua mikono yenu, ni mara ya kwanza mliyowahi kuiona. Sasa, Yesu aliahidi karama hiyo kurudi Kanisani kabla ya wakati wa mwisho.

44 Nilikuwa nikizungumza na Ndugu Demos muda mfupi uliopita kuhusu Maandiko, ambayo kama ninyi watu mngaliyajua tu, nami ninatumaini ya kwamba mnayajua, mnapowaona hawa ndugu wazuri wa haya makanisa ya kimadhehebu, Waepiskopolia, Wapresbiteri, Wamethodisti, wakija kupata *Haya*, hivi hamjui Maandiko yenu, ni jambo gani linalotukia basi? Msininii . . . Simaanishi kukemea ninaposimama hapa na kusema mambo, bali ni kwa manufaa yenu.

45 Sasa, mara niliposema hivyo, Roho Mtakatifu anaanza kutenda kazi papa hapa sasa. Ni wangapi waliowahi kuona picha hiyo? Nitakapokutana nanyi kwenye Kiti cha Hukumu, mtaona kama hili si kweli. Nuru iyo hiyo haiko futi mbili kutoka mahali ninaposimama sasa hivi. Hiyo ni kweli. Ni kitu gani? Ni Bwana aliyefufuka ambaye Paulo alikutana naye akienda zake Dameski, inaleta Uzima Wake. Afadhali niketi chini.

46 Ni wangapi ambao, kweli wanaamini hilo kwa moyo wako wote? Na—najua mliamini. Moja ya maono hayo linakufanya dhaifu kuliko kama ungesimama hapa na kuhubiri kwa saa tatu.

47 Yesu . . . Baba anapotaka kuonyesha ono . . . Sasa, wakati Lazaro alipokufa, Baba alikuwa amemwonyesha Yesu yale yatakayotukia. Sasa, kumbukeni, Yohana 5:19, Yesu alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, bali lile ambalo *amwona* Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile." Ni wangapi wanaojua ya kwamba hayo ni Maandiko? Basi Yesu Kristo kamwe hakufanya jambo moja mpaka Mungu alipomwonyesha Yeye kwanza. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo, "Si Mimi," Yeye anasema, "nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu." Sasa, tunajua hilo kuwa ni kweli; daima ni Roho wa Mungu.

48 Sasa, Yeye aliona ono la Lazaro, naye akaendelea mpaka akajua ya kwamba Lazaro alikuwa amekufa, na kusema hivyo, kisha akarudi. Kamwe hakusema jambo moja kuhusu kuwa dhaifu. Lakini maskini mwanamke mmoja aliyekuwa akitokwa na damu aligusa vazi Lake, Naye akasema, "Naona ya kwamba nguvu zimenitoka."

49 Kwa nini? Sikilizeni, enyi marafiki, wakati mmoja ilikuwa ni Mungu akitumia karama Yake kwa Lazaro, huo mwingine ilikuwa ni yule mwanamke akitumia karama ya Mungu kwa imani yake. Mnaelewa? Mnaona? Yule mwanamke, ninii yake . . . Yesu kamwe hakusema, hakugeuka na kusema, "Vema sasa, unajua ninazo nguvu, kwa hiyo nilikuponya." Alisema, "Imani yako imekuokoa." "Imani yako," imani yake ilimwokoa.

50 Sijui jinsi ningeweza kuliweka wazi zaidi kwenu, zaidi ya kusema kwamba, kwamba Mungu yuyo huyo . . . Hayuko tu hapa pamoja nami, kama Yeye angekuwa tu pamoja nami wala si pamoja nanyi, ni kwa nini kamwe lisingetukia, linahitaji mimi na wewe pamoja. Huna budi kuamini, sina budi kuamini. Nayo karama ni kama tu kuingiza, kutoka kwenye gia ndogo ukaingiza gia kubwa. Mnaona, ni kujua tu kubadilisha gia, hiyo ndiyo karama, bado ni mtu yule yule, lakini kubadilisha nafsi yako ikaingia katika Uwepo wa Mungu, na kuona tu atakayosema.

Sasa, ninajua Yeye yupo hapa. Mnaamini hilo? Iweni na imani, mtumainieni Mungu.

51 Jana ilikuwa ngumu. Ilikuwa vigumu kwangu . . . Ilikuwa ni mara yangu ya kwanza, kidogo nilikuwa na wasiwasi. Sikujua jambo hili lilikuwa karibu kutukia. Lakini kuna watu papa hapa sasa wanaoweza kuponywa. Ni wagonjwa wangapi huko nje ambao kweli, moyoni mwako, utakakubali kwamba unaomba sasa hivi? Inua mkono wako. Hakika. Mnaona? Mnaona?

52 Mama aliyeketi papa hapa, anamwombea msichana wake mdogo. Yeye ni Bibi Boggs. Huko kutokwa na damu, kama utaamini hilo kwa moyo wako wote, huko kutakoma. Unaamini, Bibi Boggs, ya kwamba mtoto wako ataponywa? Vema.

53 Ninaona Nuru ikining'inia hapa nyuma. Iko juu ya mwanamume ambaye hakika atakufa kama hana imani. Sababu ya jambo hili, kulikuwa na mwanamke jana aliyeomba dua kwa ajili ya mwanamume huyu. Ana kansa usoni mwake, naye anaomba. Bw. Peterson ndilo jina lake. Kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya. Utalikubali, Bwana? Utafanya hivyo? Simama kwa miguu yako, Mungu akubariki.

54 Mtu huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu, sijawahi kusikia habari zake, kamwe sikujua chochote kumhusu. Ikiwa—ikiwa hatufahamiani, Bwana, hata uwe nani, inua mkono wako, kama hiyo ni kweli.

Mnaamini? Ombeni tu. Ninawapa changamoto katika Jina la Yesu. Mnaona? Iweni tu na kicho kwa dakika moja, ombeni tu. Kila mtu anaomba. Aminini tu.

55 Nilidhani ilikuwa ni Florence, lakini siye, ni mwanamke mwenye umri mkubwa zaidi, ni mama yako. Sijawahi kumwona, nijuavyo mimi, maishani mwangu, hatufahamiani, lakini kati yangu na wewe amesimama mama yako. Anaingia upofu, macho

yake yana shida fulani, watoto wa macho machoni mwake; amini. Sasa, ametoweka. Sasa, Dada Shakarian, unajua siwajui wazazi wako, watu wako, sijawahi kuwaona.

56 Kuna maskini mama mmoja aliyeketi papa hapa. Ana matatizo ya kiroho anayoombea. Kidogo anaingia mvi. Mungu, usimwache aukose. Anamwombea mtu mwingine pia. Hatoki hapa, anatoka mji mwingine karibu na pwani ya bahari. Anatoka Los Angeles. Jina lake ni Bibi Pascoe, simama kwa miguu yako. Kamwe hutasumbuka tena, imani yako imekuokoa. Mungu akubariki.

Kamwe usitie shaka tena. Usitie shaka tena. Yeye yupo hapa, BWANA ASEMA HIVI.

57 Tunatoka nje muda kidogo tu, nitarudi moja kwa moja, kwa namna fulani hunipata, inarukaruka tu kila mahali, mnaona, nitarudi katika dakika moja, nitarudi moja kwa moja. [Ndugu fulani anaanza kuimba *Yote Niliyo Nayo*. Ndugu Branham anaitikia na kuanza kuvumisha—Mh.]

58 Bwana aliniambia niliporudi nyuma pale, kasema, "Omba, omba." Na—najua . . . Msifikiri nimerukwa na akili, sijarukwa na akili, najua mahali nilipo. Sasa, kama kuna mkosoaji anayetaka kukosoa, sasa ni wakati wako wa kusimama.

Maskini dada hapo kutoka Long Beach, usijali, yote yamekwisha sasa, amini.

59 Sasa, ninawatakeni mwekeane tu mikono ninyi kwa ninyi. Mungu, anayesema mambo haya, anajua yote yaliyo kweli. Hakika, Biblia . . . Mtu anaweza kuja na kunena lolote, linaweza kuwa ni la kweli au la uongo, lakini Mungu anapothibitisha kwamba ni kweli, basi hiyo ni kweli. Neno la Mungu ni kweli, mengine yote ni uongo kama ni kinyume na Neno la Mungu. Neno la Mungu lilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

60 Baba yetu wa Mbinguni, ninafanya tu hili kwa amri Yako, Bwana. Inaonekana kana kwamba yote ni kukiuka utaratibu kutoka kwa mpangilio wa kawaida, lakini ulipojongea pale pembeni, kwenye jengo, na kusema, "Rudi, ukaombe," Ninafanya tu yale uliyoniambia nifanye, Bwana.

61 Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu, wakati huu, atalitikisa kusanyiko hili hivi kwamba watatambua ya kwamba Bwana Yesu aliye hai, aliyefufuka yuko katikati yetu usiku wa leo, akitembea juu yetu, kupitia kwetu, ndani yetu.

62 Angalia, Bwana, wamewekeana mikono, nao wanamhitaji Roho Mtakatifu, wanahitaji uponyaji, shida nyingi. Hebu Mungu, Yule ambaye ndiyo kwanza anene katika maono hayo, hebu Mungu Yule aliyemfufua Mwanawe, Kristo Yesu, na amemwasilisha kwetu katika siku hizi za mwisho, jalia aje

katika nguvu za ufufuo na kumponya kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu, ampe afya kila mmoja, na kujaza na Roho Mtakatifu. Bwana, natoa ombi hili kwa kutii mapenzi Yako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

62-0129 Kuielezea Huduma
Ramada Inn
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org